# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 19  Sauli – mfalme wa kwanza

**SOMA  1 Samweli 8:19 – 22; 10:1 na 24;  13:5 – 14;  15:1 – 3 na 10 – 23**

**SOMO**

Waisraeli walipoenda kwa nchi ya ahadi, ahadi mbili kwa Ibrahimu zilitimizwa. Wazao wa Ibrahimu - Waisraeli, sasa ni **taifa** na wanaishi kwa **nchi** yao yenye Mungu aliwaahidi.

1. ***Mungu aliahidi Ibrahimu kwamba wazao wake watakuwa taifa kubwa.***
2. ***Mungu liahidi Ibrahimu kwamba atampa nchi ya Kanaani na wazao wake milele.***

Wakati Yoshua alikuwa kiongozi wao Waisraeli waliahidi kumpenda Mungu na kumtii.Walipogeuka na kuabudu miungu, Mungu aliwaadhibu. Kulikuwa na njaa na walipigwa na maadui wao. Waisraeli alipomrudia Mungu, Mungu alituma waamuzi wawasaidie na kuwafundisha njia za Mungu. Waamuzi walikuwa viongozi wa kusaidia Waisraeli lakini Mungu ndiye alikuwa Mfalme.

Waamuzi waliongoza Waisraeli kwa muda wa miaka 400. Mwamuzi wa mwisho alikuwa Samweli. Samweli alifanya bidii kwa kufundisha Waisraeli juu ya Mungu.

Samweli alipokuwa mzee, Waisraeli walimwambia kwamba wanataka mwanadamu awe mfalme wao. Hawakutaka Mungu aendelee kuwa mfalme wao. Hawakutaka waamuzi tena. Maadui wao Wafilisti, waliendelea kupigana nao. Walitaka kuwa kama mataifa mengine. Walitaka mwanadamu mwenye wanaweza kumuona awe mfalme wao. Walitaka mwanadamu kuwa kiongozi wao na aongoze jeshi lao kupigana na maadui.

Samweli alikasirika kwa sababu walitaka mfalme. Aliomba Mungu. Mungu alimwambia kwamba watu hawajamkataa yeye - walimkataa Mungu. Mungu alimwambia kwamba watapata mfalme.

**Maswali na Majibu**

*1.* Nani alikuwa mwaamuzi wa mwisho?  *Samweli*

*2.* Waamuzi walikuwa viongozi lakini nani alikuwa Mfalme?
*Mungu alikuwa ndiye Mfalme wao.*

3. Mbona Waisraeli walitaka mfalme?
*Walitaka mwanadamu wanaemuona na kuwapeleka kwa vita*.

4. Mungu alimchagua nani kuwa mfalme?  *Sauli*

*5.* Sauli alikaa namna gani?
*Alikuwa mrefu, wa sura nzuri, askari mzuri na mjasiri wa vita.*

6. Sauli alikuwa mfalme mzuri? Aliwasaidia watu kumpenda Mungu?
*Hapana. Alikuwa wa maringo na muasi. Aliongoza watu kuwa mbali na Mungu*.

7. Sauli hakumtii Mungu namna gani wakati Wafilisti walitaka kumpiga?
*Alitolea Mungu dhabihu badala ya kumwongoja Samweli*.

*8.* Sauli hakumtii Mungu namna gani wakati alikuwa akipigana na Waamaleki?
*Hakuua mfalme Agagi na aliwaweka kondoo na n'gombe wazuri*

9. Sauli alikuwa na sababu gani?
*Kwamba aliwaweka wale wanyama ili atolee Mungu dhabihu*.

10. Adhabu ya Sauli ilikuwa nini?
*Mungu alimkataa asiwe mfalme*.

## Mistari ya kukariri

1 Samweli 15:22 – 23  Mithali 28:13

## Mazungumzo

Sauli alitii amri za Mungu kiasi, mbona aliadhibiwa? Ni vyema kutii amri zingine za Mungu? Unaweza kufanya mambo mengine yenye unaona sahihi kidogo? Amri gani za Mungu unatakiwa kutii? Ni vizuri kufanya maneno mengine mbadala?

## Kuandika

Andika njia moja yenye Sauli alifanya kwa kuasi Mungu. Adhabu yake ilikuwa gani?

Samweli aliwaadharisha kwamba mfalme atachukua wana wao kuwa askari na binti wao kuwa watumishi. Lakini bado watu walitaka mfalme. Kwa hivyo aliwaachilia wawe na mfalme. Mungu aliwaachilia Waisraeli wawe na mwanadamu kama mfalme. Ingawaje Mungu ndiye alikuwa mfalme, lakini aliwapa mwanadamu kuwa mfalme – mfalme aliongoza kwa niaba ya Mungu. Mungu alichagua mfalme mwenye watu wangempenda. Alichagua mtu aliyeitwa Sauli. Alikuwa mrefu na sura nzuri. Alikuwa askari mzuri na alipigana kwa ujasiri. Samweli alimpaka mafuta ya kumtawaza Sauli kuwa mfalme wa Israeli. Halafu Samweli aliita watu wote pamoja na akawaonyesha mfalme wao mpya. Watu walipenda Sauli kwa sababu alikuwa mrefu, wa nguvu na sura nzuri. Walipasa sauti na kusema, "Mungu linda mfalme." Watu walifurahi kuwa na Sauli kama mfalme wao atakaye waongoza kupigana vita na maadui wao.

Sauli hakukuwa mfalme mzuri. Mungu hakumchagua Sauli kwa sababu alikuwa anampenda na kumtii Mungu, lakini alikuwa aina ya mtu mwenye watu walitaka. Alikuwa mrefu, sura nzuri na mwenye nguvu atakayeongoza watu kupigana vita. Sauli alipokuwa mfalme, alikuwa na maringo na kutotii Mungu. Alisababisha watu wakaacha kutii Mungu. Mungu alimpa Sauli uwezo mwingi alipokuwa mfalme. Tena alikuwa na jugumu kubwa ya kuwafundisha watu wampende na kumtii Mungu. Sauli hakuwasaidia watu kumpenda Mungu.

Wafilisti walikuwa adui wa Waisraeli. Wafilisti walikuja kupigana na Waisraeli. Sauli alikusanya majeshi ya Israeli ili wapigane na Wafilisti. Wafilisti walikuwa na nguvu sana na Waisraeli waliwaagopa. Sauli aliongoja Samweli akuje na atolee Mungu dhabihu na amuulize awasaidie kwa vita na Wafilisti. Samweli alipochelewa kukuja, Sauli hakukuwa na subira.

Wafilisti walijipanga kupigana na Wasraeli. Walikuwa na magari 30,000, watu 6,000 wa farasi na jeshi kubwa lenye halingehesabika. Waisraeli walitetemeka kwa uoga. Sauli aliogopa kwamba wanajeshi wake watatoroka. Sauli alijua kwamba ni makuhani ndio walitakiwa kutolea Mungu dhabihu. Lakini Sauli aliendelea kuwa na uoga kwa hivyo yeye mwenyewe alitolea Mungu dhabihu.



Punde si punde Samweli aliwasili. Aliambia Sauli kwamba ameasi amri za Mungu kwa yeye kutoa dhabihu. Sauli alitakiwa kuwa na imani ya kwamba Mungu angemsaidia. Mungu alimwambia kwamba kwa sababu hakumweheshimu, wana wake hawatakuwa wafalme baada yake. Ni vyema kutii Mungu **kikamilifu.**

Baadaye Mungu aliambia Sauli kuua Waamaleki wote. Mungu alimwambia Sauli kuua kila mtu hata na wanyama wao wote. Waamaleki walikuwa adui wa Waisraeli wakatili sana. Mungu alimwambia Sauli awaangamize wote. Sauli alisanya jeshi la Israeli na wakaenda kuwapiga na kuwaharibu Waamaleki.

Mungu alisaidia Waisraeli kuangamiza Waamaleki. Lakini Sauli hakuua Agagi mfalme Waamaleki. Alitaka kuonyesha ukuu wake kwa huyu mfalme. Tena Sauli aliweka kondoo na n'gombe wazuri.

Sauli aliporudi kutoka kwa vita, aliambia Samweli kwamba alikuwa ametii Mungu. Samweli alimuuliza mbona alikuwa anasikia sauti za kondoo na n'gombe wakilia. Sauli alimwambia kwamba alikuwa amewachukua kondoo na n'gombe wazuri ili awatolea Mungu kama dhabihu.

Sauli alikuwa amemuasi Mungu tena. Sasa Sauli alikuwa na majivuno. Alifikiri angemtumikia Mungu vile alitaka. Ni la maana kufanya kila kitu **sasawa** na vile Mungu anataka. Mungu hatafurahia tukifanya kinyume na matakwa yake. Mungu alitaka Sauli aue Waamaleki na wanyama wao. Lakini Sauli na watu wake waliwaacha hai mfalme na wanyama wao wazuri. Sauli alikuwa na vijisababu. Alisema eti aliweka wale wanyama ili amtolee Mungu dhabihu. Samweli aliambia Sauli kwamba heri na ya maana kumtii Mungu kuliko kutoa dhabihu.

Samweli aliamrisha mfalme Agagi wa Waamaleki aletwe kwake. Samweli alimuua Agagi vile Mungu alikuwa ameamrisha.

Sauli alikuwa na majivuno na kuasi Mungu. Alikuwa ameacha kutii Mungu tena. Samweli alimwambia Sauli, "Mungu amekukataa kwa sababu haujamtii."

Mungu alimchagua mtu mwingine awe mfalme wa Israeli.

